GREDI YA 7 - 2025

THE SCHOLAR 007

SIGNAL Publishers
Igniting thinking

# SIGNAL CBE ASSESSMENT
# JARIBIO LA SABA

## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT
## — KISWAHILI KARATASI YA 1—

**MUDA: SAA 1 DAK 30**

**JINA:** ..........................................................

**GREDI:** ..........................................................

**SHULE:** ..........................................................

**NAMBARI YA TATHMINI:** ..........................................................

**Kiapo: "Naapa kutokiuka sheria zozote wakati wa mtihani huu".**

**Sahihi:** ..........................................................  **Tarehe:** ..........................................................

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 mpaka 10.***

Familia ya mzee Kazana iliishi maisha ya umaskini mkubwa. Hata hivyo, walikuwa na watoto wawili – wa kike na wa kiume – waliothamini elimu kwa bidii ili kuonyesha shukrani kwa wazazi wao na kujiinua kimaisha. Wazazi waliwahimiza kuzingatia maadili kama vile uaminifu, utiifu, ukarimu na huruma kwa watu wote.

Siku moja, mwana wao wa kiume, Imani, aliokota kifurushi akiwa njiani kutoka shule. Alikipeleka nyumbani ili kupata ushauri wa baba yake. Baada ya kuchunguza, baba aligundua kuwa kilikuwa na mabunda ya pesa. Licha ya umaskini wao, familia ilikataa kuzitumia, bali waliamua kumtafuta mwenyewe. Habari zilipelekwa kwa chifu na hatimaye pesa zikarejeshwa kwa mfanyabiashara maarufu aliyekuwa amezipoteza akielekea benki.

Mfanyabiashara huyo alishangazwa na uaminifu wa familia ile. Alitoa shukrani kwa kuwapatia ajira mzee Kazana na mkewe, kumnunulia Imani baiskeli ya kwenda shule na dada yake viatu pamoja na vifaa vya masomo.

1. Ni kweli kusema kuwa familia ya mzee Kazana
   A. iliishi maisha ya raha mustarehe
   B. ilikuwa maskini sana
   C. ilikosa mahitaji yote
   D. ilipenda kutembea kwa majirani.
2. Familia iliyotajwa ilikuwa na watu wangapi?
   A. Wanne  B. Wawili
   C. Watano  D. Watatu.
3. Ni jambo lipi lililowafanya watoto wa familia hii wawe na bidii masomoni?
   A. Nyumbani kulikuwa na shida.
   B. Walihimizwa na wazazi wao.
   C. Walitiwa shime na walimu.
   D. Ili kuonyesha shukrani kwa wazazi.
4. Kifungu kinaonyesha kwamba elimu
   A. hupatikana kwa shida kwa wale wasio na uwezo
   B. huchangia kuwaunganisha wanajamii wote
   C. humfungulia mtu njia za kujiinua kiuchumi
   D. hufaidi zaidi waliotoka katika jamaa maskini.
5. Aya ya pili imeonyesha kuwa
   A. jamaa ya Kazana ilikuwa na shida nyingi
   B. familia ya Kazana ilizingatia mienendo ifaayo



Signal Publishers @Signal Publishers

C. majirani walishangazwa na wema wa familia hiyo
D. walimu pia walipenda Kazana kwa matendo yake.

6. Kwa nini mtoto alipeleka kifurushi nyumbani?
   A. Aligundua kwamba kilikuwa na pesa.
   B. Nyumbani kwao kulikuwa na shida nyingi.
   C. Ili baba yake apeleke kwa chifu.
   D. Alitaka kusikia maoni ya baba yake.
7. Familia ya mzee Kazana haikushawishika kutumia pesa zile kwa sababu
   A. walizoea kujitegemea kimaisha
   B. waliogopa kuchukuliwa hatua na mwenyewe
   C. waliogopa kupoteza sifa zao nzuri
   D. watoto wangelaumiwa na walimu shuleni.
8. Ni jambo lipi lililomshangaza mfanyabiashara kulingana na kifungu?
   A. Umaskini wa familia ile.
   B. Uaminifu wa familia ile.
   C. Kuzipata pesa zake.
   D. Kuwajibika kwa chifu.
9. Funzo linalojitokeza katika kifungu hiki ni kuwa
   A. ukitenda wema usingoje kulipwa
   B. mchumia juani hulia kivulini
   C. wema hauozi
   D. mchelea mwana kulia hulia yeye.
10. Neno '**uaminifu**' limetumika katika kifungu. Neno hili lina maana sawa na
    A. watiifu B. watafute
    C. wapate D. wanunue.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 11 mpaka 19.</u>***

Afya ni kutokuwa na magonjwa. Mtu asiye na afya hushindwa kushiriki shughuli za kila siku. Ili kudumisha siha njema tunapaswa kula chakula bora chenye wanga, protini na vitamini na visivyo na mafuta mengi. Kukosa lishe bora husababisha utapiamlo. Pia kila mtu anatakiwa kunywa maji safi na salama angalau glasi nane kwa siku, kwa kuwa maji machafu husababisha homa ya matumbo.

Mazoezi ya mwili ni muhimu ili kuimarisha afya, pamoja na usafi wa mwili na mazingira. Mazingira machafu huleta magonjwa kama choa na upele, na huvutia wadudu kama nzi, mbu na chawa. Aidha, pombe, sigara na dawa za kulevya husababisha maradhi kama saratani ya ini na mapafu, ilhali ngono kiholela huleta magonjwa ya zinaa kama ukimwi, kisonono na kaswende.

Kufanya kazi kupita kiasi bila kupumzika pia hudhuru afya na kusababisha maradhi ya moyo, shinikizo la damu na hata matatizo ya akili. Watu wanaotazama simu au kompyuta kwa muda mrefu hupata shida za macho. Ulaji kupita kiasi husababisha kunenepa mno kama nguruwe na maradhi ya moyo, huku kula kidogo kupita kiasi kusababisha safura na vidonda vya tumbo.

Kwa jumla, kila mtu anastahili kulinda afya yake na ya wengine, kushiriki mazoezi, kutembelea vituo vya afya, na kuzingatia kanuni zote za afya kwa kuwa afya ni bora kuliko mali.

11. Chagua jibu lililo sahihi.
    A. Mtu asiyejua kuwa ni mgonjwa huwa na afya.
    B. Mtu asiye na afya hushindwa kufanya kazi ipasavyo.
    C. Ukitaka kuwa na afya ni lazima uiname.
    D. Wenye bidii zaidi maishani huwa na afya.
12. Lishe bora huwa na virutubisho vifuatavyo isipokuwa.
    A. Wanga B. Vitamini
    C. Protini D. Mafuta mengi
13. Ugonjwa wa homa ya matumbo husababishwa na nini?
    A. Kunywa maji machafu.
    B. Maji ambayo yamechemshwa.
    C. Kutoshiriki mazoezi.
    D. Kukosa kunywa maji ya kutosha.
14. Ikiwa tutaishi katika mazingira machafu
    A. tutasambaza malaria
    B. tutapata shida za moyo
    C. tutasumbuliwa na wadudu
    D. tutaugua choa na upele.
15. Chagua ugonjwa ulio tofauti na mengine.
    A. Malaria B. Ukimwi
    C. Kaswende D. Kisonono.
16. Aya ya nne inaonyesha wazi kuwa
    A. kufanya kazi huweza kusababisha ugonjwa wa moyo
    B. shinikizo la damu huchangiwa na matatizo ya akili
    C. usipolinda afya yako utaathirika
    D. shida za macho huletwa na simu na kompyuta pekee.
17. Maneno '**<u>utanenepa kama nguruwe</u>**' yametumia mbimu gani ya lugha?
    A. Sitiara B. Chuku
    C. Nahau D. Tashbihi.
18. Mwandishi anapendekeza watu wale chakula
    A. kingi B. kifaacho
    C. kidogo D. chochote.
19. Kifungu hiki kwa jumla kinahusu
    A. utunzaji wa afya
    B. aina za magonjwa
    C. umuhimu wa mazoezi
    D. magonjwa yasiyoambukizwa.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 20 mpaka la 25.***

*(Mazungumzo baina ya Buliba na Jirani yake.)*

**Buliba:** Shikamoo baba Nanjala. Umeakaje?

**Jirani:** Marahaba. Nimeamka vyema. Naona umekuja kuzihudumia mboga zako.

**Buliba:** Naam, nahitaji kunyunyuzia maji kabla jua halijawa kali.

**Jirani:** Vijana wote wangekuwa wabunifu na wenye bidii kama wewe, mzigo wetu ungepungua.

**Buliba:** Wahenga walisema ajizi ni nyumba ya njaa. Vijana tunalo jukumu la kupambana na umaskini. Mwalimu pia husema tuanzishe miradi midogo kama huu wangu. Tukisoma kwa bidii, tutajiajiri na hata kuajiri wengine.

**Jirani:** Wewe ni kijana mwenye busara. Usikose kuwashauri wenzako. Hebu uendelee na kazi zako.

**Buliba:** Asante, baba Nanjala. Nakutakia siku njema.

20. Mazungumzo haya yalifanyika wakati gani?
    A. Jioni
    B. Mchana
    C. Adhuhuri
    D. Asubuhi.
21. Neno la heshima alilotumia Buliba katika mazungumzo haya ni
    A. naam
    B. shikamoo
    C. umeamkaje
    D. sisi vijana
22. Jirani anavutiwa zaidi na Buliba kutokana na
    A. werevu wake
    B. heshima yake
    C. mboga zake
    D. bidii na ubunifu yake.
23. Ni ushauri upi mwalimu alitoa kwa vijana?
    A. Wasome kwa bidii na pia waanzishe miradi midogo ya kujikimu.
    B. Waanzishe shughuli za kununua mahitaji ya nyumbani.
    C. Wawe na nidhamu ili wafanikiwe maishani.
    D. Wazingatie elimu yao ili wapate kazi nzuri.
24. Kwa nini Buliba aliamka mapema?
    A. Ili aende shuleni.
    B. Ili akutane na Jirani yake.
    C. Ili ashughulikie mradi wake.
    D. Ili apande mboga.
25. Methali '**ajizi ni nyumba ya njaa**' ina maana sawa na methali gani?
    A. Mtegemea cha nduguye hufa maskini.
    B. Bidii ya mja haiondoi kudura.
    C. Mwenye macho haambiwi tazama.
    D. Mkono mmoja haulei mwana.

**SAFURI**

***Jaza kila pengo katika kifungu kifuatacho kwa jawabu lifaalo Zaidi.***

Usalama katika taifa .........26......... hutegemea jinsi wananchi wenyewe.........27......... kujilinda. Kwanza ni lazima washirikiane kwani .........28.........Wananchi.........29......... ni rahisi kwao kushambuliwa. Viongozi nao wawe waadilifu.........30......... wasiwe watu wa kupokea rushwa, yaani .........31......... na kuwaachilia wahalifu. .........32......... kila familia .........33......... usalama wao kwa kufuga mbwa, kujenga ua....... 34 ......... au kuweka kamera za siri. Muhimu zaidi, kila mmoja.........35......... kuwajua walio karibu naye ili washukiwa wasijifiche miongoni mwetu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 26. A. yeyote | B. zozote | C. lolote | D. wowote |
| 27. A. wanajitahidi | B. wanavyojitahidi | C. wanapojitahidi | D. wanayojitahidi |
| 28. A. mtaka cha mvunguni sharti ainame | | B. ukiona vyaelea jua vimeundwa | |
| C. meno ya mbwa hayaumani | | D. kinga na kinga ndipo ndipo moto uwakapo | |
| 29. A. wasiposhirikiana | B. wasiyoshirikiana | C. wangeshikirikiana | D. hushirikiana |
| 30. A. ; | B. : | C. ! | D.. |
| 31. A. ada | B. nauli | C. bahashishi | D. kadhongo |
| 32. A. Lau | B. Japo | C. Isitoshe | D. Labda |
| 33. A. wajihakikishie | B. ijihakikishie | C. mjihakikishie | D. tuhakikishe |
| 34. A. thabiti | B. dhahiri | C. dhibiti | D. thubutu |
| 35. A. tujitahidi | B. wajitahidi | C. ujitahidi | D. ajitahidi |

***Kuanzia nambari 36 mpaka 50 jibu kila swali kulingana na maagizo.***

36. Chagua jibu linaloonyesha nomino ambata.
    A. Umati wa watu
    B. Mwanahewa
    C. Ubora
    D. Kucheza.

37. Bainisha sentensi iliyo katika wakati ujao hali ya kuendelea.
   A. Wachezaji watatuzwa kwa ushindi wao
   B. Bakari akija nitamwomba kitabu chake
   C. Babu atakuwa akinisimulia hadithi zake
   D. Mwalimu ameanza kufundisha
38. **Tambulisha kitenzi kishirikishi katika sentensi ifuatayo.**
   Anyango ndiye kiranja wa darasa letu.
   A. Ndiye
   B. Wa
   C. Letu
   D. Kiranja
39. **Andika umoja wa sentensi.**
   Nyanja hizo zilijengwa na serikali.
   A. Nyanja hiyo ilijengwa na serikali
   B. Uwanja huo ulijengwa na serikali
   C. Nyanja huo ulijengwa na serikali
   D. Wanja huo ulijengwa na serikali
40. **Tumia kiulizi kifaacho kujaza pengo lifuatalo.**
   Ulipougua ulitumia dawa ............?
   A. gani
   B. upi
   C. yapi
   D. mingapi
41. Alama ya kipumuo huwa na matumizi yafuatayo isipokuwa
   A. kuweka pumziko fupi katika sentensi
   B. kutenganisha maneno katika orodha
   C. kuandika tarakimu zaidi ya elfu moja
   D. kutanguliza orodha ya maneno
42. Ni nomino ipi iliyo katika ngeli tofauti?
   A. Mjusi
   B. Kilema
   C. Kipepeo
   D. Mkoba.
43. Neno lipi halijaambatanishwa ipasavyo na kinyume chake?
   A. Rafiki - hasidi
   B. Mzee - kijana
   C. Ukaidi - uaminifu
   D. Zito - jepesi.
44. Bainisha sentensi iliyo katika kauli ya kutenda.
   A. Mwima anapaka viatu rangi.
   B. Mkate huo uliokwa jana.
   C. Hawa amemchotea bibi maji.
   D. Ng'ombe watapelekewa maji.
45. Ni jibu lipi linaloonyesha sentensi ambatano?
   A. Dada anapika chakula cha jioni.
   B. Daktari anampima mgonjwa ili ajue hali yake.
   C. Wageni wote walioalikwa wamewasili.
   D. Kijumba hicho ni chake.
46. **Kanusha:**
   "Wahalifu hao walitiwa mbaroni"
   A. Wahalifu hao hawajatiwa mbaroni
   B. Wahalifu hao hawatiwi mbaroni
   C. Wahalifu hao hawakutiwa mbaroni
   D. Wahalifu hao hawatatiwa mbaroni
47. Ngoma ni kwa kigoma kama vile jani ni kwa;
   A. Kijijani
   B. Kijani
   C. Jijani
   D. Majani
48. **Kamilisha;**
   Vijana hao wangeshauriwa ................ waadilifu.
   A. walikuwa
   B. watakuwa
   C. wangekuwa
   D. wangalikua.
49. Ni sentensi ipi iliyo na kivumishi cha sifa?
   A. Gari jipya limenunuliwa.
   B. Nguo zao ni safi.
   C. Kabati hili ni lake.
   D. Mkono ambao unauma ni huu.
50. Nahau ipi imeambatanishwa vizuri na maana yake?
   A. Paka tope - kumsifu mtu sana.
   B. Piga jeki - shirikiana kufanya jambo.
   C. Tia mrija - saidia mtu kufanya jambo.
   D. Unga mkono - kubaliana na maoni ya mtu.